

**MOROGORO URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORITY  
(MORUWASA)**



MORUWASA

**MORUWASA SACCOS LIMITED**  
P.O. Box 5476, Morogoro, Telephone: +255 654369810  
Email: [saccos@moruwasa.go.tz](mailto:saccos@moruwasa.go.tz),



**TANGAZO LA ZABUNI YA KUKODISHA CANTEEN (MGAHAWA) KWA  
AJILI YA KUTOA HUDUMA YA CHAKULA ILIYOPO KWENYE JENGO  
LA MAKAO MAKUU YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA  
MAZINGIRA MOROGORO (MORUWASA)**

**NAMBA YA TENDA: MORUWASACOS/P/CANT/2023/01**

Mwenyekiti wa SACCOS ya MORUWASA (MORUWASA SACCOS LTD), anawatangazia Wazabuni/Makampuni/Wajasiliamali/Ushirika/Vikundi/ au Wananchi wenye uwezo wa kukodi Canteen kwa ajili ya kutoa huduma ya Chakula iliyopo jengo la Makao makuu ya MORUWASA, Morogoro.

**MASHARTI YA MUOMBAJI**

1. Muombaji awe ni raia wa Tanzania.
2. Muombaji aambatanishe kivuli cha leseni ya Biashara.
3. Muombaji aambatanishe kivuli cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN Certificate).
4. Muombaji aambatanishe kivuli cha taarifa za Kampuni (Company profile kwa makampuni tu).
5. Mwombaji (kama atahitaji kuona eneo la kutolea huduma), afike ofisi ya SACCOS iliyopo MORUWASA Makao makuu.
6. Mwombaji atakayepata kazi hii atawajibika kulipia bili ya umeme na maji kulingana na atakavyoelekezwa.
7. Mwombaji ataje kiasi cha fedha atakacholipa MORUWASA SACCOS kwa mwezi (Malipo ya pango kwa mwezi) na malipo haya yatafanyika mwanzoni mwa Mwezi (kwa Miezi Sita) katika akaunti namba ya SACCOS.
8. Gharama za Usafi kwenye eneo la biashara ni jukumu lake mwenyewe.
9. Mwombaji awe na vyombo vya kutosha kufanyia kazi.
10. Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha (samani) kama viti, meza, kabati za kuhifadhia chakula n.k vitakavyomwezesha kuhudumia Wateja kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

11. Mwombaji atatakiwa kufika ofisi ya SACOSS MORUWASA kabla ya kulipa ada ya maombi ili kupata fomu ya orodha ya vyakula vinavyotakiwa ili mwombaji ajaze bei kabla ya kutuma maombi.
12. Mwombaji awe tayari kupikia chakula kwenye jiko la Canteen na si chakula kutoka nje ya eneo la MORUWASA.
13. Mwombaji hataruhusiwa kutumia kuni wakati wa maandalizi ya chakula cha Wateja.
14. Mwombaji ataje uzoefu na sifa zake zote katika maombi ya kazi anayoomba.
15. **Mwombaji azingatie Usafi wa chakula, wahudumu, mavazi husika ya watoa huduma, vyombo nk.**
16. **Endapo Mwajili hataridhika na mwenendo wa huduma inayotolewa na Mzabuni atasitisha mkataba wakati wowote.**
17. **Mwombaji atakayepata kazi hii ahakikishe Wafanyakazi wake wana vyeti vya kupima afya (Medical Examination Certificate).**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA NI KAMA IFUATAVYO;**

- I. Mwombaji atatakiwa kulipa Ada ya Maombi Tshs. 50,000/= (Elfu Hamsini tu.), baada ya kupata fomu ya orodha ya vyakula kutoka ofisi ya MORUWASA SACCOS. Hivyo Mwombaji anatakiwa kulipa kiasi hicho kwenye akaunti Namba **00111509785801** yenye jina la MORUWASA SACCOS na *Deposit Slip* ya benki iwasilishwe sambamba na barua ya maombi. **Fedha hizo hazitarudishwa.**
- II. Maombi hayo yanatakiwa yatumwe kwenye bahasha iliyofungwa kwa **lakiri** ikiwa na barua ya maombi pamoja na fomu ya orodha ya vyakula iliyojazwa bei.
- III. Bahasha ya Maombi itumwe kwa: Mwenyekiti wa Bodi ya SACCOS MORUWASA, S. L. P. 5476 MOROGORO.
- IV. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 29/09/2023 saa 9:00 JIONI na zabuni zitafunguliwa katika Ofisi ya Ugavi na Manunuzi MORUWASA kuanzia saa 9:30 JIONI siku hiyo hiyo. Waombaji/ wawakilishi wote wa Zabuni watakaopenda kushuhudia funguzi huo wanakaribishwa kuhudhuria.

22 Sept, 2023

CPA Dagrás G. Gwahila  
**MWENYEKITI – BODI YA SACCOS MORUWASA**

